Stanbic
Bank




# Karibu Stanbic Bank

# Stanbic
# Visa Debit Card






Fanya malipo kwa urahisi ukitumia Kadi yako ya Stanbic Visa Debit, ambayo hutoa urahisi wa kufikia akaunti yako papo hapo na kwa njia salama wakati wowote. Kadi ya Stanbic Debit Visa inakubaliwa ulimwenguni pote, mteja anaweza kutoa fedha kupitia ATM zozote zinazokubali kadi ya VISA na pia kufanya malipo kupitia POS zozote zinazokubali kadi za VISA kwenye maduka ya Wafanyabiashara na malipo ya Mtandaoni.

**Kwa nini Stanbic Visa Debit Card?**

Zinakubalika kote ulimwenguni, na zinatoa ufikiaji wa haraka, salama na rahisi wa pesa kwenye akaunti yako ya benki ili kufanya malipo mtandaoni, ng'ambo na kwa kupitia simu kwa urahisi.

Kuna wepesi wa kutumia Kadi ya Stanbic Visa Debit kwenye mifumo yoyote ya ATM, POS, na biashara mtandao inayokubali Kadi za benki za Visa.

**Jinsi ya kufanya malipo kupitia kadi ya Stanbic Visa Debit**

- Tumia kadi ya Stanbic Visa Debit kwenye POS, fanya malipo mtandaoni au toa pesa kwenye ATM.
- Furahia uwezekano usio na kikomo na urahisi ukiwa na Kadi ya Stanbic Visa Debit ili ufanye malipo popote, kwa chochote, na wakati wowote mtandaoni.
- Fanya manunuzi mtandaoni kutoka kwenye tovuti au App yoyote ikijumuisha Amazon, BestBuy, eBay na AliExpress.
- Jisajili kwenye chaneli za filamu ikiwa ni pamoja na Netflix, HBO, Amazon Prime na Showmax.
- Nunua huduma zozote za App unazotaka kutoka Google Playstore na Apple Store.
- Fanya manunuzi ya tiketi za ndege mtandaoni ukitumia Kadi yako kwenye shirika lolote la ndege duniani kote.
- Weka miadi ya malazi kutoka kwa hoteli ulimwenguni kote kupitia Booking.com, Hotels.com, Expedia na Airbnb.
- Unganisha Kadi yako ya Stanbic Visa Debit na PayPal ili kufanya malipo kwa urahisi na usalama zaidi.
- Furahia punguzo kutoka kwa wauzaji unapofanya miamala ya POS kulingana na matangazo yanayoshirikishwa kwenye mifumo yetu, mitandao ya kijamii, barua pepe, SMS na matangazo ya redioni.




## Platinum Visa Debit Card

- Furahia ufikiaji wa bure kwenye sehemu maalum za mapumziko kwenye uwanja wa ndege ndani na nje ya nchi.
- Bima - Ubadilishaji wa kadi bila malipo, Ulinzi wa manunuzi, Udhamini wa manunuzi ulioongezwa
- Ongezeko la thamani - Ufikiaji bila malipo kwenye sehemu maalum ya mapumziko ya hadi watu 4 iwapo kuna ucheleweshwaji wa safari ya ndege, mwenye kadi atatimiza masharti ya kutumia huduma hii hadi mara 8 kwa mwaka.

*Vigezo na Masharti kuzingatiwa

Tupigie **BURE**: **0800 751111 |** Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com** | www.stanbicbank.co.tz

Stanbic
Bank



# Ndoto ya kujenga himaya yako inaanza na akaunti ya Stanbic **WEZESHA™**

**Akiba | Bima | Mkopo |**

Tualike kwenye ofisi zako kwa maelezo zaidi, au tembelea tawi la benki lililo karibu nawe

**Changanua Msimbo wa QR uwasiliane na Kai sasa.**

+255 742 000 636

# Karibu **Tukuwezeshe**

## Sifa za akaunti

1. Upatikanaji wa bure wa bima ya mazishi kwa ajili yako na familia yako
    - Faida za bima ya mazishi kwa mwenye akaunti, mwenzi wake na Watoto
2. Utoaji bure wa fedha kwenye kaunta bila makato kwa kiasi kifikacho hadi TZS 10 Milioni
3. Kuhamisha fedha ni bure kutoka akaunti moja Kwenda akaunti nyingine za ndani ya benki ya Stanbic
4. Upatikanaji wa ufadhili wa malipo ya bima
5. Upatikanaji wa bure wa suluhisho rahisi za uwekezaji
    - Akaunti ya Contrasave
    - Unit Trust of Tanzania – UTT
6. Upatikanaji wa ushauri wa kifedha na uwekezaji kupitia program yetu ya mafunzo ya ustadi wa kudhibiti fedha
7. Upatikanaji wa kadi binafsi za benki mara moja baada ya ombi
8. Upatikanaji wa Smart App yetu, USSD na Benki Mtandao
9. Upatikanaji wa mawakala wetu wa Stanbic nchi nzima
10. Mkopo kianzio wa hadi TZS milioni 5
11. Upatikanaji wa haraka wa mkopo kulingana na hitaji lako
12. Unapata huduma pendelevu kutoka kwa mshauri wako wa masuala ya kibenki akisaidiwa na kitengo chetu cha mawasiliano cha wateja
13. Huduma zetu zinakufuata ulipo pale unapoweka ombi

Vigezo na Masharti kuzingatiwa

Tupigie **BURE**: **0800 751111 |** Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com** | www.stanbicbank.co.tz

Stanbic Bank

# Mkopo wa Gari



Hili ni suluhisho lililoundwa maalum kwa ufadhili wa muda mfupi hadi wa kati ili kufadhili ununuzi wa mali zinazohamishika, kama vile magari na mashine.

Tupigie **BURE**: **0800 751111**
Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com**
www.stanbicbank.co.tz

**Ufadhili wa gari la kibinafsi ni pamoja na:**
**Mpango wa gari la mtu binafsi:**
**Ukodishaji wa kifedha:** Hii huturuhusu kununua mali na kuikodisha kwa wateja kwa malipo mahususi ya kukodisha. Wateja wanaweza kutuma maombi ya huduma hii kulingana na mapato ya kila mwezi. Chaguo pia linapatikana kwa wahamiaji halali wanaofanya kazi nchini kwa muda ambao haujaisha katika mkataba wao kwa zaidi ya miaka miwili.

**Miradi ya magari ya kampuni:**
**Ufadhili wa moja kwa moja:** tunafadhili waajiri kwa shughuli za kawaida au kwa msingi wa kukodisha (kukodisha kifedha). Kisha mwajiri humpa mfanyakazi haki ya kutumia gari.

**Mpango hakiki:** tunatoa fedha kwa wafanyakazi na mwajiri wao hutuhakikishia kuwa atafanya makato ya kila mwezi kutoka kwa mshahara wa mfanyakazi wao. Mwajiri huhakikisha kwamba malipo yote yametimizwa huku mfanyakazi akiendelea kubaki na kampuni na anahakikisha utatuzi wa mikataba yote ya fedha.

**Mpango simamizi:** tunatoa fedha kwa wafanyakazi huku mwajiri akitoa usaidizi wa kiutawala kupitia makato ya kila mwezi kutoka kwa mshahara wa mfanyakazi na hutufahamisha kuhusu kujiuzulu na kuachishwa kazi.

**Vigezo vya VAF kwa Mtu Binafsi, wamiliki pekee na kampuni**

- Kufadhili gari binafsi jipya na lililotumika
- Kwa magari mapya: yawe mapya hadi miezi 6 baada ya kusajiliwa.
- Kwa magari binafsi yaliyotumika: kuanzia miaka 12 (aina nyingine za magari) hadi miaka 15 (magari ya Toyota) tangu tarehe ya kutengenezwa.
- Kwa magari ya biashara: yasizidi miaka 8 tangu tarehe ya kutengenezwa.
- Uwiano wa makato ya mkopo dhidi ya mapato ni 60% kwa waajiriwa. Kwa wamiliki wa biashara, uwezo wa kulipa utazingatia taarifa za fedha zilizofanyiwa tathmini (AFS).
- Kiasi cha juu cha ufadhili wa benki ni 90% ya bei ya ankara ya kodi kwa gari jipya na 70% ya thamani ya soko kwa gari lililotumika
- Mchango wa mteja hadi 30% kwa magari yaliyotumika na 10% ya ankara/manunuzi ya kodi ya gari mpya
- Muda mrefu Zaidi wa ulipaji ni hadi miezi 84 kwa gari jipya na miezi 60 kwa gari lililotumika
- Mkopo una ulinzi binafsi, dhamana ni gari linalofadhiliwa, ambapo kadi ya gari inabaki chini ya uhifadhi wa benki katika kipindi chote cha mkopo
- Ufungaji wa kifaa cha kufuatilia kwenye gari linalofadhiliwa.
- Bima ya hadhi ya juu kwa ajili ya gari linalofadhiliwa.

**Mahitaji ya watu wanaolipwa mshahara:**

- Fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu (imeambatanishwa)
- Taarifa ya kibinafsi iliyokamilishwa ya mapato na matumizi na mizania (kielelezo kimeambatishwa)
- Uthibitisho wa mapato (Payslips)
- Uthibitisho wa ajira(mkataba wa ajira)
- Uthibitisho wa makazi (Barua kutoka kwa Mtendaji wa Kata, bili ya matumizi, uthibitisho wa mwajiri, mkataba wa kukodi / kukodisha au mkataba wa mkopo wa nyumba wa benki)
- Uthibitisho wa kitambulisho (pasipoti au leseni ya kuendesha gari au vitambulisho vya kitaifa na kibali cha kazi kwa asiye mkazi)
- Angalau taarifa ya benki ya miezi sita kwa wateja wasio wa benki ya Stanbic, walio na akaunti benki nyingine.
- ankara ya mauzo kutoka kwa wauzaji gari linalopendekezwa kufadhiliwa.
- Mwajiri kuandika barua ya kuelekeza mshahara wa mfanyakazi kwenye akaunti ya benki ya Stanbic na pia barua ya uwezeshaji (kielelezo kimeambatishwa)

**Mahitaji ya Mmiliki Pekee na ya Kampuni**

- Nakala zilizothibitishwa za;
  a. MEMART
  b. Mapato ya hivi karibuni ya kila mwaka
  c. Vyeti vya usajili wa TIN na VAT
  d. Certificate of incorporation
  e. Dondoo la jina la Biashara (mmiliki pekee)
  f. Kitambulisho cha wakurugenzi

- Barua ya maombi ya mkopo
- Azimio la Bodi
- Mpango wa biashara
- Taarifa ya Benki ya miezi 12
- ankara ya malipo
- Orodha ya mikataba
- 3years Ukaguzi wa fedha
- Makadirio ya kifedha ya miaka 3
- Akaunti za usimamizi zilizohakikiwa mpaka hivi karibuni
- Ripoti safi ya idara simamizi ya mikopo/madeni.

Tupigie **BURE**: **0800 751111**
Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com**
www.stanbicbank.co.tz

Stanbic Bank

# **Mkopo** wa nyumba

Furahia kumbukumbu za kudumu katika nyumba ndoto yako

Bei nafuu | Rahisi | Kwa haraka



Tupigie **BURE**: **0800 751111**
Au barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.co.tz**

**Mkopo wa kufanikisha ununuzi wa nyumba kwa hadi 90% ya gharama:** Kulingana na malengo yako na thamani ya nyumba husika, Benki ya Stanbic Tanzania itakupatia mkopo wa hadi 90% ya bei ya mauziano.

**Mkopo wa uboreshaji wa makazi:** Kwa kulingana na thamani ya sokoni ya nyumba yako, Benki ya Stanbic Tanzania itakuwezesha kupata mkopo lingani wa hadi 75% ili kufanikisha malengo yako ya uboreshaji hali.

**Mkopo wa rehani ya nyumba:** Je, unajua unaweza kurejesha kwa urahisi sehemu ya gharama iliyotumika wakati wa ununuzi au ujenzi wa nyumba yako kupitia mkopo wa rehani? Benki ya Stanbic imekuletea utaratibu wa kipekee unaokuwezesha kupata hadi 75% ya thamani ya nyumba yako ili kufanikisha malengo yako mengine ya kifedha.

## Nani anaweza kuomba mkopo wa nyumba?

Wakazi na wasio wakazi (diasporas) Watanzania wenye umri zaidi ya miaka 18 ambao ni;

- Waajiriwa, mtu binafsi au pamoja na mwenza (mke au mume),
- Wamiliki wa biashara,
- Vyanzo vingine vya mapato vinaweza kuzingatiwa*

## Maelezo ya jumla ya mkopo

- Muda wa juu zaidi wa kurejesha mkopo wa hadi miaka 20
- Riba shindani
- Kiwango cha juu cha mkopo kwa mkopaji mmoja cha hadi TZS bilioni 1.2 (kiasi lingani kwa fedha ya kigeni USD),
- Mapato ya pamoja; Benki ya Stanbic itakokotoa kiasi cha mkopo stahiki kulingana na asilimia ya mapato yenu ya kila mwezi kwa ujumla,
- Benki ya Stanbic itafanya ukaguzi wa historia ya ukopaji wako kabla ya kushughulikia ombi lako
- Utahitajika kuwa bima dhidi ya mkopo husika (credit protection) na thamani ya nyumba (property insurance) kwa kipindi chote cha urejeshaji,

## Gharama za ziada kuzingatiwa

- Kiwango cha chini asilimia 10 ya bei ya mauziano (hitaji hii halitahusisha mikopo ya rehani)
- Ada ya mara moja kwa mkopo husika isiyozidi 1.8%,
- Ada ya uthamini wa nyumba,
- Ada za gharama za kisheria za usajili wa hati katika wizara ya ardhi,
- Bima dhidi ya thamani ya nyumba (property insurance) - 0.15%,
- Bima dhidi mkopo husika (credit protection) – ulemavu wa kudumu na kifo,

## Vielelezo vinavyohitajika

**Jumla (aina zote)**

- Fomu ya maombi ya mkopo iliyojazwa kwa usahihi na kwa kuzingatia vigezo na masharti,
- Mkataba wa mauziano,
- Nakala ya utambulisho wa kitaifa, pasipoti au leseni ya udereva,
- Picha 2 za ukubwa wa pasipoti saizi,
- Nakala ya hati miliki,
- Ripoti ya uthamini wa nyumba (Benki ya Stanbic itakupa orodha ya watathimini mali kwa chaguo lako)

**Muombaji mwajiriwa**

- Fungua akaunti ya mshahara Benki ya Stanbic Tanzania,
- Nakala za malipo ya mshahara kwa miezi mitatu iliyopita/ uthibitisho wa mapato,
- Taarifa ya akaunti ya msharaha kutoka benki husika za miezi 12 ya nyuma (kama mshahara unapita benki nyingine),
- Nakala zilizoidhinishwa na mwajiri juu ya taarifa binafsi za mwajiriwa,
- Nakala ya mkataba wa ajira,
- Barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiri wako
- Nakala ya kitambulisho cha kazi

**Waombaji wa Diaspora**

- Fungua akaunti ya miamala na Benki ya Stanbic Tanzania,
- Nakala za malipo ya mshahara wako kwa miezi mitatu iliyopita /ushahidi wa mapato,
- Nakala zilizoidhinishwa za taarifa binafsi za benki kwa miezi 12 (kutoka nje ya nchi),
- Nakala ya pasipoti halali ya Kitanzania,
- Kibali cha kiserikali cha ufanyaji kazi kutoka nchi husika,
- Barua ya utambulizho kutoka kwa mwajiri wako,

**Waliojiajiri/Wamiliki wa biashara**

- Taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa miaka mitatu,
- Taarifa za benki za miezi 12 kwa akaunti za biashara na uthibitisho wa mapato kutoka kwa mkaguzi,
- Azimio la bodi (dhamana ya ulipaji wa mkopo kwa mkurugenzi anayeomba mkopo),
- Nakala iliyoidhinishwa ya MEMARTS kwa wamiliki/ wakurugenzi wa makampuni
- Nakala iliyoidhinishwa ya cheti cha kusajiliwa kwa wamiliki/wakurugenzi wa kampuni
- Nakala iliyoidhinishwa ya cheti cha usajili & dondoo kutoka kwa msajili - ikiwa kuna ushirikiano wa kibiashara uliosajiliwa
- Maelezo kina ya biashara husika (juu ya dhamira, maono, mikataba mikuu, muundo wa shirika, mipango ya ukuaji na urithi)
- Nakala ya cheti cha utambulisho wa mlipakodi (TIN) na/ au cheti cha usajili wa VAT
- Nakala ya cheti cha kibali cha mlipa kodi
- Nakala ya leseni halali ya biashara
- Uchunguzaji usajili wa BRELA



Tupie **BURE**: **0800 751111**
Au barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.co.tz**
**www.stanbicbank.co.tz**

Stanbic Bank



# Ndoto hutimia
# **weka akiba kuzitimiza**

Turuhusu tuwe njia ya mafanikio yako kupitia orodha ya bidhaa mbalimbali zilizoundwa kukusaidia kuweka akiba ili ufikie ndoto zako pamoja na faida itakayopatikana kulingana na akiba na muda ulioweka akiba husika.

**Contract Save | Pure Save | Fixed Deposit**

Tupigie **BURE**: **0800 751111**

# Akaunti za Akiba
# Pata Faida kutokana na akiba yako!

## Akaunti ya Contract Save

Hii ni akaunti ya uwekezaji inayokusaidia kuweka akiba kwa lengo maalum kwa kipindi kinachobadilika kuanzia mwezi 1 hadi miezi 60.

Madhumuni ya akaunti hii ni kuwasaidia wateja kuwa na mpango wa bei nafuu wa kuweka akiba unaolenga kukidhi mahitaji yao mahususi. Ni bora ikiwa unataka kuweka akiba kwa gharama kubwa za siku zijazo kama vile amana ya nyumba, sherehe ya harusi, ada ya shule, n.k.

Agizo la kudumu la kila mwezi linahitajika kutoka kwa akaunti yako kuu kwenda akaunti ya mkataba ya akiba ili kuhakikisha kuwa akaunti ina pesa katika kipindi chote pamoja na njia za ziada za kuweka amana kama vile kwa Mawakala wa benki, Machine za kuwekea pesa (CDM).

### Sifa za akaunti

- Inapatikana kwa TZS
- Kiwango cha chini cha amana cha kufungua Akaunti cha TZS 20,000
- Uondoaji hauruhusiwi; fedha haziwezi kutolewa wakati wa kipindi cha uwekezaji.

### Faida za akaunti

- Pata riba isiyobadilika kwa mwaka (makato ya WHT yatahusika)
- Riba huhesabiwa kila siku na kulipwa kila mwezi
- Kipindi cha uwekezaji kinachobadilika kuanzia mwezi 1 hadi miezi 60.
- Hakuna ada za kila mwezi za usimamizi
- Maagizo ya utaratibu wa kufanya hamisho la fedha kutoka akaunti kuu Kwenda akaunti ya akiba bila malipo
- Kuweka Amana bure ukiwa kaunta ya tawi la benki, Machine ya kuweka pesha (CDM) & WAKALA
- Hamisha pesa bure kutoka USSD, Internet banking na App na uongezee amana yako
- Hamisha Kutoka benki zingine na uongeze amana yako kwenye contract save account
- Taarifa za SMS bila malipo kwa miamala ya kifedha ya akaunti.
- Hakuna Kadi inayotolewa
- Uwezo wa kuhamisha akiba yako mwishoni mwa kipindi chako cha kuhifadhi Kwenda kwenye akaunti nyingine yoyote
- Unaweza kuwa na zaidi ya akaunti moja kwa malengo yako tofauti ya kuweka akiba

### Stahiki na nyaraka

- Awe na umri wa miaka 18 au zaidi
- Awe na akaunti tayari na sisi
- Picha 1 kubwa ya pasipoti
- Cheti cha TIN
- Fomu ya maombi iliyojazwa

## Akaunti ya Pure Save

Akaunti hii ya akiba inakupa fursa ya kukuza pesa zako kwa mahitaji ya siku zijazo. Ukiwa na akaunti ya Pure Save, Riba hulipwa kwa kiwango na huongezeka kadiri salio linavyoongezeka. Pesa zinapatikana zinapohitajika na kiasi chochote kinaweza kuwekwa wakati wowote.

### Sifa za akaunti

- Inapatikana kwa TZS, USD, EUR, GBP, ZAR
- Kiwango cha chini cha kufungua akaunti na salio la uendeshaji
- Upataji wa riba kwa akaunti ya TZS & USD pekee
- Salio la Chini la Kupata riba TZS 100,000 & USD 100
- Hakuna kikomo cha kuweka au kutoa (ada ya kutoa itahusika)
- Hakuna kadi iniyotolewa
- Gharama zingine za miamala ni kulingana na Mwongozo wa Ushuru wa Stanbic

### Faida ya akaunti

- Hakuna ada ya kila mwezi ya usimamizi ikiwa salio la akaunti liko juu Kiwango cha chini cha kufungua akaunti na salio la uendeshaji (TZS 20.000, EUR,USD,GBP 100 & ZAR 300)
- Toa pesa mara moja kwa mwezi bila malipo kwenye kaunta, zaidi ya hapo mteja atatozwa
- Riba hutolewa kwa viwango na huongezeka kadiri salio linavyoongezeka
- Riba kulipwa kila mwezi na huongezeka kulingana na salio lililopo kwenye akaunti
- Upatikanaji wa njia za kidigitali (USSD, APP, Internet banking)
- Akiba inaweza kuongezwa wakati wowote - urahisi katika kuweka amana.
- Hakuna kikomo cha kutoa fedha

### Stahiki na nyaraka

- Picha 1 ya pasipoti
- Kitambulisho Halali (NIDA)
- Cheti cha TIN
- Uthibitishaji wa anwani ya makazi inayokubalika.
- Kwa wageni (pamoja na hayo hapo juu): Kibali halali cha makazi / kazi iliyoidhinishwa na Pasipoti Halali
- Fomu ya maombi iliyojazwa

## Akaunti ya Fixed Deposit

Akaunti ya uwekezaji ambayo inakupa fursa ya kuwekeza kwa masharti maalum (Kiasi, Kiwango cha Riba na Muda).

Vipindi vya uwekezaji vinapatikana kuanzia mwezi 1 hadi miezi 36. Amana isiyobadilika hutoa viwango vya riba vya juu kuliko akaunti za kawaida za akiba.

Mteja hupewa urahisi wa kujadili kiwango cha riba kulingana na kiasi cha amana na uhitaji wa wakati huo.

### Sifa za akaunti

- Inapatikana kwa TZS, USD, EUR, GBP, ZAR
- Salio la chini kabisa la kufungua akaunti TZS 500 000 & EQV katika FCY
- Riba hupatikana kwa akaunti za TZS & USD pekee
- Muda wa kukaa kati ya mwezi 1 hadi 36
- Uondoaji fedha hauruhusiwi; fedha haziwezi kutolewa wakati wa kipindi cha uwekezaji.

### Faida za akauti

- Hakuna ada za kila mwezi za usimamizi
- Viwango vya ushindani vya riba (Viwango vya riba vinapatikana kwa ombi katika matawi yote).
- Ombi la riba: Riba inaweza kulipwa kila mwezi, robo mwaka, kila mwaka au kikomo
- Urahisi wa kuchagua tarehe ya umiliki na ya kikomo
- Unaweza kuwa na akaunti ya amana zaidi ya moja ikiwa ungependa kuweka akiba kwa malengo tofauti
- Pesa katika akaunti hii zinaweza kuwekwa rehani na kutumika kama dhamana

### Stahiki na nyaraka

- Awe na umri wa miaka 18 au zaidi
- Kuwa na akaunti tayari na sisi ya uendeshaji
- Cheti cha TIN
- Fomu ya maombi iliyojazwa

Stanbic Bank



# Weka Akiba kwa urahisi, tumia kwa akili

**Akaunti ya Universal ya Stanbic imebuniwa kwa ajili ya wafanyakazi wa msimu kama wewe.**

## Faida Unazopata:

- Hakuna ada ya mwezi
- Pata riba kila mwezi kwenye akiba yako
- Weka au toa pesa muda wowote popote ulipo
- Upatikanaji wa huduma saa 24 kupitia ATM, App, Mtandao & Wakala
- Kadi ya Visa kwa malipo ya papo kwa papo na ununuzi wa mtandaoni
- Fursa ya kutumia akaunti hata ukiwa Kenya, Uganda au Sudan Kusini

## Kwa Nini Hii Akaunti ni Muhimu:

Kama unafanya kazi kwenye kilimo, ujenzi, biashara au utalii, mapato yako yanahitaji sehemu salama ya kuyahifadhi na kuyakuza.

## Mahitaji Rahisi ya Kujiunga:

- Picha ndogo moja ya pasipoti
- Kitambulisho halali (NIDA)

**Tembelea tawi la Stanbic au WAKALA aliye karibu nawe kujiunga leo!**

Piga Bure: **0800 751 111** | **www.stanbicbank.co.tz**


Stanbic Bank
Msomi Account
Changanua Msimbo wa QR
Fungua
Akaunti ya Msomi
papo hapo
Barua pepe: msomiaccount@stanbic.co.tz

# Akaunti ya Msomi

Akaunti hii ni bidhaa ya kipekee ambayo hutolewa kwa wanafunzi wa umri kati ya miaka 18 hadi 27 ili kuwasaidia kufanya miamala binafsi ya gharama nafuu na kuweka historia nzuri ya kifedha.

Akaunti hii inatoa njia rahisi na nafuu kwa wanafunzi kupokea, kutuma na kupata fedha zao kutoka nchi yoyote wanaposoma. Wanafunzi wanaweza kutumia akaunti zao kulipia ada, dharura na malipo mengine ya KADI na POS.

**Sifa na Faida za akaunti**

- Inapatikana kwa Sarafu ya TZS na USD
- Unapata Kadi ya Visa kwa gharama nafuu
- Upatikanaji wa huduma binafsi za kidigitali (Internet, App na Mobile Banking)
- Taarifa za SMS bila malipo kwa miamala ya kifedha ya akaunti.
- Fanya miamala ya Kutoa, Kuweka au Uhamisho wa pesa ukiwa Kenya, Uganda na Sudan ya Kusini
- Upatikanaji wa akaunti 24/7 kupitia ATM na STANBIC Wakala

**Stahiki & Nyaraka ili kuwa na akaunti**

- Lazima awe mwanafunzi mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 27.
- Picha moja (1) ya hivi karibuni ya pasipoti.
- Nakala ya kitambulisho halali: Kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa wanafunzi wenye miaka 18 na kuendelea au Kitambulisho cha Mkaazi wa Zanzibar.
- Kitambulisho halali cha Chuo au Chuo Kikuu.
- Barua ya udahili kutoka Chuo au Chuo Kikuu.

**Huduma nyingine za faida**

- Unapata huduma mahususi za Kadi ya VISA na punguzo za bei unapofanya miamala maalum
- Program yetu ya mafunzo ya ustadi wa kudhibiti fedha
- Fursa kwenye majukwaa ya kazi, warsha na programu za kujifunza kudhibiti fedha na usimamizi wa pesa

**Makato**

- Salio la chini la ufunguzi na uendeshaji akaunti: TZS 5,000 & USD 10
- Hakuna makato ya kila Mwezi ya usimamizi wa akaunti yako
- Utoaji wa bure wa fedha kwenye ATM za Stanbic

Stanbic Bank

# Hekima ni

tabasamu la kustaafu



Haina makato ya mwezi

Pata riba

Pata punguzo

Programu za afya

Mipango ya kustaafu

Ushari wa mali

Bima

Pata mkopo

**HEKIMA BANKING** inakuwezesha kupata mkopo wa hadi **TZS 80,000,000** wenye riba nafuu kama mstaafu. Fao lako ndio dhamana kuu kwenye mkopo huu.

Piga **BURE**: **0800 751111**

Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com** | **www.stanbicbank.co.tz**

## HEKIMA BANKING

Hii ni akaunti maalum kwa mahitaji ya kibenki kwa wale walio na umri wa miaka 55 na zaidi. Akaunti hii imeundwa kwa ajili ya watu ambao tayari wamestaafu au watastaafu hivi karibuni, ili kukidhi mahitaji yao mahususi ikiwa ni pamoja na kufanya miamala, kuweka akiba, uwekezaji na huduma za ushauri wa kifedha ili kuhakikisha unastaafu kwa starehe.

## SIFA ZA AKAUNTI

- Inapatikana kwa TZS, USD, EUR, GBP, ZAR
- Haina ada za kila mwezi
- Haina salio la chini la uendeshaji akaunti
- Gharama zingine za kufanya miamala ni kulingana na Mwongozo wa Ushuru wa Benki ya Stanbic

## FAIDA ZA AKAUNTI

- Upataji wa Mkopo wa Wastaafu
- Mpango mkakati wa kustaafu, Huduma za Ushauri wa Uwekezaji na kukuza mali
- Inastahiki kadi za benki za VISA (ada ya Kadi Mpya inahusika)
- Bima ya matibabu (kwa ombi) na bidhaa nyingine za bima
- Matumizi ya akaunti masaa 24/7 kupitia ATM, SimBanking, Internet banking & STANBIC Wakala

## MAELEZO ZAIDI KUHUSU MKOPO WA HEKIMA

Akaunti ya Hekima inakuwezesha kupata mkopo wa hadi TZS 80,000,000 wenye riba nafuu kama mstaafu. Fao lako ndio dhamana kuu kwenye mkopo huu.

## FAIDA ZA MIKOPO YA WAASTAFU

- Unaweza kukopa kiasi chochote kuanzia Tsh. 500,000 mpaka kufikia Tsh. 80,000,000.
- Muda wa mkopo hadi miaka 7 (miezi 84).
- Mikopo inapatikana kwa urahisi katika matawi yote ya Stanbic.
- Ni mkopo wenye Bima ambayo itakukinga na majanga kama kifo na ulemavu wa kudumu.
- Riba nafuu ambayo hutozwa katika salio la mkopo.
- Mkopaji hapangiwi lengo la mkopo.
- Mteja hatakiwi kuweka dhamana yoyote ila Mfuko wa hifadhi husika utahakikisha malipo ya pensheni ya mstaafu yanalipwa na kuendelea kupita katika akaunti ya Stanbic katika kipindi chote cha mkopo.
- Hakuna gharama za uendeshaji wa Akaunti ya Mstaafu.
- Unapata faida ya kila mwezi kutokana na amana zalizopo kwenye akaunti yako.
- Unaweza pata mkopo Mkubwa kwa makato madogo kwaajili ya kutimiza malengo yako.
- Benki inaweza nunua mikopo ya taasisi nyingine. Unaruhusiwa nyongeza ya mkopo (Top Up)

## SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na akaunti Stanbic na pensheni yake ipitie kwenye akaunti hiyo.
- Nakala ya kitambulisho cha mstaafu au Nakala ya kadi ya uanachama ya Mfuko wa hifadhi ya jamii.
- Nakala ya historia ya malipo ya pensheni ya kila mwezi kutoka kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii.
- Picha 1 ya passport size
- Kielelezo kinachokubalika cha kuhakiki makazi: Barua kutoka serikali ya mtaa kama umehama makazi

Piga **BURE**: **0800 751111**
Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com**
www.stanbicbank.co.tz



Stanbic Bank

# **Vikundi** Akaunti

Huduma hii ni maalum kwaajili ya mahitaji ya kibenki ya vikundi rasmi na visivyo rasmi kama vile VICOBA, Wajasiriamali wadogo wadogo, vikundi vya dini, vikundi vya wafanyakazi na wanafamilia.

Piga bure: **0800 751111**
Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com**
www.stanbicbank.co.tz

## VIKUNDI AKAUNTI

Huduma hii ni maalum kwaajili ya mahitaji ya kibenki ya vikundi rasmi na visivyo rasmi kama vile VICOBA, Wajasiriamali wadogo wadogo , vikundi vya dini, vikundi vya wafanyakazi na wanafamilia. Hivi ni vikundi binafsi vinavoundwa na watu wasiopungua watano wenye malengo ya kusaidiana katika masuala mbalimbali ya kijamii na kifedha.

## FAIDA ZA KUFUNGUA VIKUNDI AKAUNTI

- Kiwango nafuu cha kufungulia akaunti.
- Haina makato ya mwezi.
- Haina makato ya kuweka fedha
- Akaunti yenye riba kwa mwezi.
- Usalama na uhakika wa fedha zako.
- Huduma ya kibenki masaa 24 kupitia mawakala na ATM.
- Wanachama kuweza kuweka pesa kwenye akaunti ya KIKUNDI muda wowote masaa 24 zilipo machine za kuwekewa pesa.
- Kupata taarifa za akaunti kwa njia ya kidigitali bure.
- Elimu ya kifedha na uwekezaji bure kwa kikundi.
- Kupata meneja mahusiano mwenye uelewa mkubwa wa kibenki na vikundi.

## UTARATIBU WAKUFUNGUA AKAUNTI

- Barua ya Serikali za mitaa.
- Katiba ya kikundi
- Vitambulisho vya taifa vya wanachama wote
- Picha za paspoti za viongozi na watia sahihi wateule wa benki.
- Muhtasari wa kikundi unaoainisha jina la kikundi, makubaliano ya kufungua akaunti benki ya Stanbic, orodha ya wanakikundi wote na nyadhifa zao, orodha ya watia sahihi wa benki (Walau watia sahihi wawili-2). Muhtasari unapaswa kusainiwa na idadi ya wanakikundi kwa mujibu wa katiba yao.
- Fomu ya kufungua akaunti iliyojazwa.
- Shilingi za kitanzania 50,000-kianzio cha kufungulia akaunti.

## UWEKEZAJI

**Kikundi kitafurahia urahisi wa akaunti zetu za kuwekeza zenye riba nzuri inayovutia.**

- Akaunti ya kuwekeza kwa muda mrefu: Akaunti hii inakuhakikishia faida kwakupitia riba zetu shindani.
- Kupitia Stanbic Biashara Incubator unapata fursa za mafunzo ya uongozi,kodi, sheria, mikataba, masoko, manunuzi, usimamizi wa fedha, Biashara na urasimishaji wa Biashara, kuunganishwa na masoko mbali mbali nchini na nje ya nchi.

## BIMA

**Upatikanaji wa huduma bora za bima mbalimbali za vikundi**

- Mkono wa pole: Tunatoa mkono wa pole endapo mwanachama akafariki au kufiwa na mwenza, Watoto mpaka wanne, wazazi pamoja na wakwe.
- Bima ya Elimu: Bima hii ni kwa ajili ya Elimu Pamoja na mipango mingine uliyoipanga kwa ajili ya mtoto pale mwanachama atakapopatwa na janga la kifo au ulemavu wa kudumu litakalomsababishia kushindwa kumudu shughuli zake za kuingiza kipato, Bima hii itaenda kuwapa fidia wategemezi kuweza kukamilisha mipango iliyoyokwa na mzazi kabla ya majanga.
- Bima kwa miradi mbalimbali ya kikundi na wanachama binafsi; mali za biashara, usafirishaji, ofisi za Biashara, Kilimo na ufugaji.
- Bima ya Afya kwa wanachama: Bima hii inaenda kumlinda mwanachama kwa kushughulikia/kulipa gharama za matibabu.
- Bima Binafsi kwa wanachama: Bima ya vyombo vya moto, Nyumba na samani za ndani, vifaa vya umeme n.k

Piga **BURE**: **0800 751111**
Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com**
www.stanbicbank.co.tz



# Akaunti ya Pamoja

## Maono ya Pamoja, Utajiri wa Pamoja.

Hii ni akaunti ya benki iliyoundwa kwa ajili ya watu wawili kusimamia fedha pamoja- inayofaa wanandoa, familia, washirika wa biashara au marafiki walio na malengo ya pamoja ya kifedha.

### Vipengele

- Inapatikana kwa Sarafu ya TZS, USD, EUR, GBP na ZAR
- Inafunguliwa kwa Kiwango cha chini cha amana
- Inakupa uwezo wa kuongeza fursa na kuwekeza katika akaunti zetu za akiba au uwekezaji
- Kiwango cha riba cha ushindani kinatolewa kwenye akaunti kulingana na Malengo ya uwekezaji
- Inakuwezesha kufanya miamala kupitia njia za kielektroniki
- Uwezo wa kupata Kadi ya malipo ya VISA kwaajili ya miamala zaidi
- Ina Ada ya usimamizi wa kila mwezi kwa akaunti ya hundi na za akiba
- Gharama zingine za miamala ni kulingana na Mwongozo wa Gharama wa Stanbic

### Manufaa: Kwanini uchague akaunti yetu ya Pamoja?

- Usimamizi: dhibiti fedha zako kwa pamoja katika akaunti moja
- Udhibiti wa Fedha wa Pamoja: mamlaka ya kutia sahihi kwa matumizi ya akaunti (Mmoja kutia saini, ama yoyote kutia sahihi au wote wawili kutia sahihi)
- Urahisi: Fikia akaunti yako wakati wowote kupitia mifumo yetu ya kidijitali ukiwa na uwezo wa kufanya miamala na kulipa kwa pamoja bili zako.
- Uwazi na Uaminifu: wamiliki wote wa akaunti wana uwezo wa kupata taarifa ya miamala yote kupitia mfumo salama wa kidijitali ili kujenga uwajibikaji na uaminifu.
- Akiba inayotokana na malengo: Pata zaidi kwenye akaunti ya uwekezaji inayolenga kulipa mahitaji ya baadaye ya gharama za familia, kupanga harusi, ada ya shule n.k.
- Benki bila mipaka: Uwezo wa kupata Huduma ya kibenki bila mipaka ndani ya Kenya, Uganda na Sudan Kusini

### Kustahiki na Mahitaji


- Wateja lazima wawe na umri wa miaka 18 au zaidi
- Uthibitisho wa Kitambulisho halali (kwa pande zote)
- Picha moja (1) ya saizi ya pasipoti ya hivi karibuni (kwa wahusika wote)
- Fomu ya maombi ya kufungua akaunti ya pamoja iliyojazwa na kusainiwa

Piga BURE 0800 751111

Stanbic Bank

Pata Bima kupitia Stanbic Bank

# Tupo kwa Ajili yako



Bima ya Gari

Bima ya Nyumba

Bima ya Afya

Bima ya Safari

Bima ya Maisha

Bima ya Elimu

Tupigie **BURE**: **0800 751111**

Washirika wetu wa Bima

Alliance Life Assurance | Alliance Insurance | Jubilee General Insurance | Allianz | Britam – With you every step of the way | Heritage Insurance Co Tanzania – "With us …rest assured…" | UAP | Mayfair Insurance | Sanlam – Live with confidence | Strategis Insurance

#BimaBomba

## Je Wajua?
Gharama ya Matibabu ndiyo sababu kuu ya changamoto za kifedha nchini Tanzania.

Pata Bima yako ya afya kupitia Stanbic benki kitengo cha Bancassurance kutoka kwa washirika wetu bora wa bima ya afya.

- Utalipiwa gharama za matibabu na ada ya kumuona daktari
- Familia yako itahakikishiwa huduma ya matibabu ikitokea hali ya ugonjwa wa ghafla.
- Upatikanaji wa watoa huduma kwa saa 24.
- Upatikanaji wa mtandao mkubwa wa mahospitali bora nchini Tanzania

## Hakikisha Elimu ya Mtoto wako
Hakuna sababu ya elimu ya mtoto wako kukatizwa ukipata ulemavu wa kudumu au kufariki.

Pata mpango wako wa bima ya elimu kupitia  kitengo cha Bancassurance kutoka kwa washirika wetu bora wa bima ya maisha.

- You will ensure that your child will access quality education.
- Reduce financial burden by saving for higher learning.
- Take care of your children's educational needs and expenses even after you pass away.
- Get a flexible premium payment plan for the scheme.

## Ni wakati wa kulinda gari lako
Hakuna haja ya kuwa na wasiwasi gari lako linapohusika katika ajali.

Katia bima ya gari kupitia Stanbic Bancassurance kutoka kwa washirika wetu bora.

- Nyumba yako itajengwa tena ikiharibiwa kwa moto au majanga mengine ya asili.
- Kurekebishiwa mandhari ya nyumba yako baada ya kuharibiwa na moto.
- Malazi mbadala baada ya ajali kutokea
- Kulipia gharama ya kikosi cha zima moto endapo ajali ya moto itatokea.

## Safiri kwa amani
Pata faraja ya kulipwa baada ya kupoteza mzigo wako.

Pata Bima yako ya Safari kupitia Stanbic Bancassurance kutoka kwa washirika wetu bora wa bima.

- Kurejeshewa gharama zako za matibabu unapougua kwa dharula nje ya nchi.
- Kurejeshewa gharama uliyotumia kunapokuwa na kuchelewa kwa safari ya ndege.
- Kurejeshewa gharama za hati zilizopotea kama vile Pasipoti.
- Pata malipo ya mzigo uliopotea wakati wa safari.

Stanbic Bank

# MSINGI WA MAISHA YAO HUJENGWA SASA

- Furahia viwango vinono vya riba
- Okoa gharama kwa kutoa pesa bure mara moja kwa mwezi katika matawi yetu
- Fanikisha matarajio yao ya badae kwa kufanya standing order bure kila mwezi
- Unapata Kadi ya Visa yenye chip na pin
- Hakuna makato ya mwezi ikiwa kiwango kwenye akaunti yako hakijashuka
- Mafunzo na warsha mbali mbali ya kujifunza kifedha na usimamizi wa pesa



Piga **BURE**: **0800 751111**
Barua pepe: **tanzaniaccc@stanbic.com** | **www.stanbicbank.co.tz**

Stanbic Bank



Je, wewe ni Mtumishi wa Umma?

# Unahitaji Mkopo?

Pata hadi **TZS Milioni 300**
Papo hapo kupitia **eMkopo!**

**Haraka. Bila Makaratasi. Kwa Watumishi wa Umma**

Mtumishi wa umma, je umewahi kujikuta ukihitaji mkopo wa haraka kwa ajili ya ujenzi, ada za shule, kuongeza mtaji wa biashara au gharama za dharura?

Kupitia eMkopo wa benki ya Stanbic, kupata mkopo ni rahisi kuliko hapo awali. Hakuna makaratasi, hakuna kusubiri matawini – yote ni kidijitali, kupitia **Watumishi Portal.**

## How to kuomba:

1. Tembelea: **https://ess.utumishi.go.tz**
2. Chagua **Stanbic Bank**
3. Weka kiasi cha mkopo unachotaka

## Faida za eMkopo

- Kopa hadi TZS milioni 300 papo hapo
- Bila makaratasi wala foleni benki
- Masharti rahisi, riba nafuu
- Muda wa urejeshaji  hadi miezi 132 (miaka 11)
- Fedha huingia moja kwa moja kwenye akaunti yako kwa haraka
- Tunanunua mikopo kutoka kwa taasisi nyingine za fedha

**Mkopo Wako. Kinamna Yako.**

Huduma hii ni mahsusi kwa Watumishi Wa Serikali.

Kwa msaada zaidi: Piga simu BURE **0800 751 111** au au tembelea tawi la Stanbic lililo karibu.

Stanbic Bank



# Huduma za kibenki kokote

1 Kupitia SmartApp / Intaneti Benki




https://www.stanbicbank.co.tz/tanzania/personal

***150*29#**

Standard Bank / Stanbic Bank

GET IT ON Google Play

Download on the App Store

2 Kupitia Stanbic Bank Wakala




- Weka / Toa Pesa
- Lipa Bili na kodi
- Fungua Akaunti

Fanya miamala, Pata mikopo, hamisha pesa kutoka akaunti moja kwenda nyingine, au fanya malipo kama vile: **TanQR na Lipa Namba, Lipa bili za DAWASA, LUKU, Ving'amuzi na Malipo ya GePG**. kwa urahisi, haraka na usalama! Yote haya yanawezekana moja kwa moja kutoka kwenye akaunti yako kupitia: Stanbic App, Intaneti Benki na Wakala wa Stanbic. Au kwa urahisi kupitia USSD ***150*29#**

Stanbic Bank



# Benki Zaidi ya Mipaka

## Huduma ya Kibenki Isiyo na Mipaka ukanda wa Afrika Mashariki na Stanbic Bank.

Sasa unaweza kufurahia huduma za benki kwa urahisi katika nchi hizi; **Uganda, Kenya, Tanzania na Sudan Kusini** kupitia mtandao wa kanda wa Stanbic Bank.

**Pata pesa zako. Popote. Wakati wowote.**

**Unachoweza Kufanya:**

- **Kuweka na kutoa** pesa taslimu kwa sarafu ya ndani au ya kigeni
- **Kuhamisha fedha kuvuka mipaka**
- **Kukagua akaunti yako** kutoka nchi yako ya nyumbani
- Kufanya miamala **kwenye tawi** au **kupitia Intaneti Benki**
- **Kufikia fedha zako papo kwa hapo**

**Benki Moja. Nchi Nne. Urahisi Kamili.**

# Matawi yetu Tanzania

Tuna matawi 16, vituo 3 vya huduma na zaidi ya Mawakala 448 ndani ya mikoa yote nchini.

**Tawi la Center**
Makao Makuu ya Benki
Kona ya Barabara
ya Ali Hassan Mwinyi
na barabara ya Kinondoni
P.O. Box 72647, Dar es Salaam
Tel: 255 22 2666430

**Tawi la Main**
Jengo la IT Plaza
Mtaa wa Ohio, Posta
P.O. Box 72647, Dar es Salaam
Tel: 255 22 2113742

**Tawi la Peninsula**
Barabara ya Haile Selassie
Masaki mwisho
P.O. Box 6437, Dar es Salaam
Tel: 255 22 2184940 - 42

**Tawi la Kariakoo**
Mtaa wa Narung'ombe
P.O. Box 72647, Dar es Salaam
Tel: 255 22 2113742

**Tawi la Industrial**
Jengo la GSM
Barabara ya Nyerere
P.O. Box 9992, Dar es Salaam
Tel: 255 22 286562 – 3

**Tawi la Moshi**
Block 10GIII
Boma Road
P.O. Box 9992, Dar es Salaam
Tel: 255 27 2754409/483

**Tawi la Arusha**
Sokoine Drive
P.O. Box 3062, Arusha
Tel: 255 27 2509713/6

**Tawi la Mbeya**
Lupa way/ Barabara ya Karume
P.O. Box 147, Mbeya
Tel: 255 25 200380/81

**Tawi la Mwanza**
Jengo namba. 14 Block
Barabara ya Makongoro
na Mtaa wa Ghana
P.O. Box 3064, Mwanza
Tel: 255 28 2500 948/473

**Tawi la Dodoma**
Jengo namba 1, Block K
Mtaa wa Mbeya
P.O. Box 22327, Dodoma
**Tawi la Tanga**
Block KBII Central Area
Barabara ya Independence
P.O. Box 730, Tanga

**Tawi la Geita**
Otonde Plaza, Geita

**Tawi la Ubungo**
Plot Na. P28792, EACLC – Manispaa ya Ubungo

**Tawi la Karatu**
Block G, Plot Na. 1300, Mtaa wa TFA, Mji wa Karatu

**Tawi la Kahama**
Plot Na. 153, Block B, Eneo la Mjini Kahama, Shinyanga

**VITUO VIDOGO VYA HUDUMA**
**Mbeya**
Kabwe – Mwanjelwa Viwandani
Barabara ya Tunduma
na barabara ya Kabwe

**Mwanza**
Barabara ya Nyerere,
Mtaa wa Libert, Mongo House

**Arusha**
Majengo – Mtaa wa Elerai,
Barabara ya Dodoma

**Kituo cha Huduma cha Arusha Kwa Mromboo Biashara Centre**
Plot Na. 1, Block A,
Kituo cha Mafuta cha Kwa Mrombo Afroil,
Mlimani, Jiji la Arusha

**Kituo cha Huduma cha Tegeta Biashara Centre**
Kibo Commercial Complex,
Block E, Tegeta

**Kituo cha Huduma cha Dar Village Biashara Centre**
Dar Village Mall, Plot Na. P32115,
Garden Road, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam

**KWA MAELEZO ZAIDI**
**Huduma kwa wateja**

**Nambari ya bure**
Wateja Binafsi na Wakubwa 0800 751 111
Wateja wa CIB 0800 751 020
Wateja wa Biashara 0800 751 021

**Barua pepe**
tanzaniaccc@stanbic.com
www.stanbicbank.co.tz

**MUDA WA KAZI**
**Tawi la Kariakoo**
**Jumatatu - Jumamosi**
Saa 2.30 Asubuhi - Saa 1 Usiku

**Jumapili na Sikukuu za Kitaifa**
Yamefungwa

**Matawi mengine**
**Jumatatu - Ijumaa**
Saa 2 Asubuhi - Saa 10 Jioni

**Jumamosi**
Saa 2.30 Asubuhi - Saa 8Mchana

**Jumapili na Siku za Sikukuu**
Yamefungwa

Stanbic
Bank